**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEM**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0768445510**

**Makamu Mkuu wa Shule**

**0712713791/ 0711718432**

**Patron 062868509**

**Shule ya Sekondari Mbweniteta**

**S.L.P. 67337,**

**Dar es salaam**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MBWENITETA HALMASHAURI YA KINONDONI MKOA DAR ES SALAAM MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Mbweniteta ipo kata ya MBWENI umbali wa Kilometa 04 kutoka barabara kuu kufika shuleni. Kwa wanafunzi wanaotoka mikoani ukishuka kituo cha mabasi ya mkoa (Magufuli)panda daladala za kwenda **Tegeta nyuki** ukifika panda

daladala za **Mbweni**. Kama unatokea hapa hapa Daar-es-salam, fika stendi ya **Makumbusho** au **Mawasiliano** na ukishafika **Makumbusho** au **Mawasiliano** shuka halafu panda daladala za kwenda **Mbweni** na utashuka kituo kinachoitwa **Ubungo**, mkono wa kushoto utaona barabara ya lami tembea utafika shule ni mwendo wa kilometa 1. Pia Kwa wanafunzi wanaotokea ARUSHA, MOSHI na TANGA shuka Kituo kinaitwa BOKO MAGENGENI panda pikipiki nauli 1500 au panda bajaji nauli 4000, ama panda daladala la mbweni nauli sh. 500/=

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 03/07/2023, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 02/07/2023.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Suruali 02 rangi ya **Dark blue** yenye marinda 02 na mkunjo wa chini (turnup), isiwe ya kubana.
ii. Mashati meupe 02 ya mikono mirefu.
iii. Fulana nyeupe 02
iv. Sare ya Michezo ni bukta 01 na fulana 01 dark blue ya chelsea.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino.
vi. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta 01 dark blue inapatikana karibu na shule
ix. Nguo za kushindia baada ya masomo ni suluali 02 nyeusi, Track sut dark blue pair 01 kwaajili ya kujisomea usiku.
x. Tai 02 dark blue zinapatikana karibu na shule.
xi. Tisheti ya 01 ya kijivu (form six) itavaliwa siku ya jumanne na ijumaa ambayo inapatikana karibu na shule.
xii. T-sheti 02 nyekundu za shingo ya duara isiyo na maandishi ambazo zinapatikana karibu na shule.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 07 counter book Quire 4.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Spring files 03 za kutunzia mitihani, majaribio na taarifa muhimu.
iv. Vitabu vya masomo utapewa ushauri na walimu wa masomo shuleni.
v. Begi 01 jeusi la mgongoni la kubebea madaftari

vi. Scientific Calculator kwa tahasusi ya HGL.
vii. Godoro lenye ukubwa wa size ya 31/2
viii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue, foronya ya godoro 1 na chandarua 01.
ix. Pazia moja rangi ya blue bahari kwa ajili ya dirisha la chumba chako
x. Nguo za ndani za kutosha;
xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xii. Ndoo 2. Ndogo 01 (lita Kumi) na kubwa o1( lita ishirini) zenye mifuniko.
xiii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje. Vinapatikana karibu na shule.

**ANGALIZO**: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa aina yoyote ile.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro na kutokuandika nukuu za masomo.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni. Unyoaji wa kiduku/panki ni marufuku kwa mwanafunzi.
vii. Kufuga ndevu;

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kutoroka au kwenda nje ya eneo la shule bila Ruhusa ya mwalimu.
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule Alphonce Peter Sway**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0768 445 510**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0712 713791/ 0711718432**
- **Mwandamizi Taaluma 0655 152 558**
- **Mwandamizi Malezi 0716 670 867**